HOTUBA YA MGENI RASMI, MHESHIMIWA DKT. HUSSEIN A. MWINYI (MB), WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII KATIKA SHEREHE YA MAADHIMISHO YA MIAKA KUMI (10) YA MAMLAKA YA CHAKULA NA DAWA (TFDA) TAREHE 17 OKTOBA, 2013

Mheshimiwa Dkt. Seif S. Rashid (Mb), Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii,

Mheshimiwa Margareth Sitta (Mb), Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii,

Mheshimiwa Anna Abdallah (Mb), Mbunge wa Viti Maalum,

Bwana Charles Pallangyo, Katibu Mkuu, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii,

Bwana George Yambesi, Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma,

Waheshimiwa Mabalozi na Wawakilishi wa Mashirika ya Kimataifa,

Dkt. Donan Mmbando, Mganga Mkuu wa Serikali

Mwenyekiti na Wajumbe wa Bodi ya Ushauri ya Wizara ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa TFDA,

Bwana Hiiti B. Sillo, Mkurugenzi Mkuu wa TFDA,

Wakuu wa Taasisi za Serikali na asasi zisizo za kiserikali,

Viongozi wa Serikali,

Wakurugenzi na watumishi wa TFDA,

Waandishi wa Habari,

Wageni waalikwa,

Mabibi na Mabwana,

Napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa sote tulioko hapa zawadi kubwa ya uhai na afya njema kwa siku ya leo. Vilevile napenda kutoa shukrani kwa Bodi ya Ushauri ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa TFDA na Menejimenti ya TFDA kwa kunipa heshima ya kuwa mgeni rasmi katika sherehe hii ya kutimiza miaka kumi tangu Serikali iunde chombo hiki muhimu kwa taifa letu.

Ndugu Wafanyakazi,

Ninaamini kwamba kila mmoja wetu anaguswa na kazi zinazofanywa na Mamlaka hii kutokana na kwamba sisi sote tunatumia bidhaa wanazozisimamia angalau kila siku. Hivyo, Serikali inapoona taasisi hii inazidi kukua na kujiimarisha inafarijika kwa sababu tutaendelea kuwa na uhakika wa kupata bidhaa salama, bora na zenye ufanisi unaotarajiwa za chakula, dawa, vipodozi na vifaa tiba.

Ndugu wafanyakazi,

Maelezo ya awali yaliyotolewa na Katibu Mkuu, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na Mkurugenzi Mkuu wa TFDA yameonesha mafanikio mengi ambayo Mamlaka imeyapata katika kipindi cha miaka kumi.

Serikali inatambua juhudi zinazofanywa na TFDA katika kujenga mifumo ya udhibiti wa bidhaa ambayo ndio msingi wa mafanikio yalioainishwa. Baadhi ya mafanikio ni pamoja na maabara yenu kukidhi vigezo vya umahiri vya Shirika la Afya Duniani (WHO Prequalification), ithibati kwa viwango vya ISO kwa maabara na mifumo ya udhibiti wa dawa na chakula, kuanzishwa kwa Ofisi tano za Kanda na kuanzishwa na kusambaza Mpango wa Maduka ya Dawa Muhimu nchini. Mafanikio haya yanaonesha jinsi ambavyo TFDA imedhamiria kuboresha udhibiti wa bidhaa katika kipindi kifupi cha miaka kumi.

Hivyo, napenda kuipongeza Bodi ya Ushauri ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa TFDA (MAB), Menejimenti na wafanyakazi wa Mamlaka ya Chakula na Dawa kwa mafanikio haya.

Ndugu wafanyakazi,

Ninapenda kuwapongeza sana Menejimenti na wafanyakazi kwa moyo wa kizalendo kwa kujitoa kwenu kuchangia madawati 100 yaliyotolewa kwa shule za msingi jirani na TFDA za Makuburi na Makuburi Jeshini. Ninaamini moyo huu wa upendo uliowezesha wafanyakazi kuchangia jumla ya Tzs 7,600,000/= kutoka kwenye mishahara yenu itakuwa chachu kwa wanafunzi hao kujiendeleza katika masomo yao ili waje kuwa viongozi wa baadaye na taifa letu. Aidha, naipongeza Menejimenti kwa kuchangia Tzs 10,000,000/= kama sehemu ya mchango wa taasisi kwa jamii (corporate social responsibility) na hivyo kuwezesha madawati hayo 100 kutengenezwa.

Vile vile nawapongeza kwa ubunifu wa kutunga wimbo wa kuhamasisha jamii kushiriki mapambano dhidi ya dawa bandia ambao maudhui yake yanaendana na kauli mbiu ya miaka kumi ya TFDA isemayo “kwa pamoja tupambane na bidhaa duni na bandia ili kulinda afya zetu”. Hongereni sana. Aidha, nazipongeza timu zilizoshinda katika michezo mbalimbali na hivyo kupata vikombe.

Ndugu wafanyakazi,

Mafanikio mliyoyapata yawe chachu ya kuongeza ufanisi kiutendaji ili kufikia dira mliyojiwekea ya kuwa Mamlaka inayoongoza Barani Afrika katika udhibiti wa ubora na usalama wa chakula, dawa, vipodozi na vifaa tiba kwa wote. Mkifikia dira hiyo mtakuwa mmetekeleza kikamilifu jukumu mlilopewa na Serikali la kulinda afya ya jamii. Serikali ina imani kuwa mnao uwezo wa kuwa taasisi bora ya udhibiti duniani kwani hakuna kizuizi cha kufikia dira hii.

Nimefurahishwa sana na uamuzi wenu wa kuweka kumbukumbu ya miaka 10 ya TFDA kwa kuandika kitabu chenye mafanikio katika udhibiti wa chakula, dawa, vipodozi na vifaa tiba. Nimeelezwa kwamba kitabu hicho kinaainisha historia ya udhibiti hapa nchini, mafanikio yaliyopatikana katika miaka 10 ya TFDA na changamoto zilizopo. Wito wangu ni kusambaza kitabu hicho kwa wadau wote muhimu

ili wafahamu historia ya udhibiti ili watoe mchango stahiki kwa kipindi kingine cha miaka 10 ya TFDA.

Ndugu wafanyakazi,

Serikali inatambua ugumu wa kazi za udhibiti kutokana na mabadiliko ya sayansi, teknolojia, falsafa, mahitaji makubwa ya rasilimali, mabadiliko ya tabia na mahitaji ya jamii na kuwepo kwa mifumo tofauti ya udhibiti duniani. Kwa kutambua hali hii, Serikali kupitia Wizara yangu itaendelea kuhamasisha na kushirikiana na wadau katika kuijengea TFDA uwezo zaidi katika kuhimili changamoto hizo. Aidha, Serikali itaendelea kusimamia utekelezaji wa makubaliano ya kisera katika Jumuiya za kikanda na kimataifa zenye lengo la kuimarisha udhibiti na vilevile kuweza kutumia fursa zilizopo.

Serikali itaendelea kuboresha mazingira yenu ya kazi kila itakapowezekana na kusaidia upatikanaji wa rasilimali zinazohitajika ili muweze kutekeleza majukumu yenu kwa ufanisi zaidi. Hii ni pamoja na kuhakikisha upatikanaji wa rasilimali watu na fedha za kununua vitendea kazi na uendeshaji.

Ndugu wafanyakazi,

Napenda kutumia fursa hii kuwaomba wananchi kutoa ushirikiano kwa TFDA hasa katika kutoa taarifa pale wanapokuwa na shaka kuhusu bidhaa fulani au pale wanapohisi kwamba kuna bidhaa ambazo zimetengenezwa chini ya viwango. Kufanya hivyo kutaiwezesha Mamlaka kubaini kwa urahisi bidhaa duni na bandia kwenye soko na hivyo kuzuia madhara yanayoweza kutokea.

Nimeona ni vyema nikumbushe jukumu hili la jamii hasa kwa vile uzoefu uliopo duniani unaonesha kuwa wananchi wana nafasi kubwa katika kuisaidia Serikali katika kudhibiti ubora na usalama wa bidhaa.

Napenda vilevile, kutoa shukrani za dhati kwa Wizara, taasisi za kiserikali na zisizo za kiserikali na wadau wa maendeleo

kama alivyowataja Mkurugenzi Mkuu wa TFDA kwa mchango wenu mkubwa kwa maendeleo ya Mamlaka.

Ndugu wafanyakazi,

Nirudie kutoa shukrani na pongezi nyingi kwenu kwa mafanikio makubwa mliyoyafikia. Sina shaka kuwa mtaendelea kuwa mfano mzuri kwa taasisi nyingine za umma hapa nchini. Hivyo, dumisheni mafanikio haya ili mlinde heshima na taswira ya TFDA kwa wananchi na taifa kwa ujumla. Aidha, endelezeni ushirikiano na wadau katika kutekeleza majukumu mliyopewa na Serikali.

Tumieni fursa hii ya maadhimisho ya miaka kumi kutafakari na kupanga mikakati ya kuzibadili changamoto zilizopo kuwa fursa za kuimarisha utekelezaji wa majukumu yenu. Ni wazi kwamba vita iliyoko mbele yetu bado ni kubwa na kwa misingi huu hiyo unahitajika ubunifu na jitihada za makusudi za kila mfanyakazi wa TFDA katika kuhakikisha ushindi unapatikana katika vita hii. Katika dunia ya sasa ni mwiko kufanya kazi kwa mazoea bali kila wakati tujiulize; kuna njia ipi bora zaidi kuleta ufanisi? Kwani wengi wanaofanikiwa ni wale wanaofanya mambo ya kawaida kwa njia tofauti.

Ndugu wafanyakazi,

Napenda kutoa rai kwa Bodi ya Ushauri, Menejimenti na wafanyakazi wa TFDA katika kipindi cha miaka kumi ijayo kujielekeza katika maeneo yafuatayo;

i. Kuongeza mtandao wa udhibiti hadi ngazi ya Halmashauri;
ii. Kuimarisha utoaji wa elimu kwa jamii;
iii. Kuimarisha udhibiti wa vyakula visivyosindikwa;
iv. Kuimarisha udhibiti wa dawa asili na tiba mbadala;
v. Kuimarisha udhibiti wa vitendanishi (in vitro dignostics); na
vi. Kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli kwa lengo la kujenga uwezo wa kujitegemea kifedha.

Ndugu wafanyakazi,

Napenda kuhitimisha hotuba yangu kwa kuwaomba kila mdau kutoa mchango wake katika kuhakikisha kuwa chakula, dawa, vipodozi na vifaa tiba ni bora na salama ili kulinda afya zetu.

Ni matarajio yangu kwamba baada ya miaka kumi ijayo, TFDA itakuwa imejiimarisha kiutendaji hadi ngazi ya Wilaya na vile vile katika ngazi ya kikanda na kimataifa ili kufikia dira yake ya kuwa taasisi inayoongoza barani Afrika katika kudhibiti usalama, ubora, ufanisi wa chakula, dawa, vipodozi na vifaa tiba kwa wote.

Ahsanteni sana kwa kunisikiliza.